SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# Matokeo ya Viashiria Muhimu

## 2019/20 Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi


**Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali**
**Wizara ya Fedha na Mipango**
**Zanzibar**



**Semptemba, 2020**

## Dira

Dira ya Ofisi ni kuwa “Kitu cha ubora kwa ajili ua uzalishaji wa takwimu rasmi na kukuza utamaduni wa kutumia ushahidi wa kitakwimu ili kuweza kuandaa sera na kufanya maamuzi”.

## Dhamira

Dahamira ya Ofisi ni kuratibu uzalishaji wa takwimu rasmi, kutoa takwimu na taarifa zenye ubora wa hali ya juu na kuhamasisha matumizi yake katika mipango, kufanya maamuzi, utawala, uendeshaji, ufuatiliaji na tathmini.

Kwa maoni na ushauri, tafadhali wasiliana na nasi;
Mtakwimu Mkuu wa Serikali,
Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali,
P.O. Box 2321,
Zanzibar
Tel: +255 24 2231869
Fax: +255 24 2231742
Email: zanzstat@ocgs.go.tz
Website: www.ocgs.go.tz

# YALIYOMO


**YALIYOMO** ... iii
**Orodha ya Jadweli** ... v
**Orodha ya Michoro** ... vi
DIBAJI ... vii
**SHUKRANI** ... viii
**UTANGULIZI** ... 1
1.0 Muhtasari ... 1
1.1 Malengo ya Utafiti ... 2
**2.0 UTEKELEZAJI WA UTAFITI** ... 3
2.1 Muundo wa Sampuli ... 3
2.1.1 Mbinu za Utafiti ... 3
2.1.2 Mgawanyiko na Ukubwa wa Sampuli ... 3
2.2 Maboresho ... 4
*Mabadiliko ya kimuundo* ... 4
*Ongezeko la moduli au maswali* ... 4
2.3 Madodoso ... 5
2.4 Utafiti wa Majaribio ... 6
2.4.1 Majaribio ya Awali ... 6
2.4.2 Majaribio ... 6
2.5 Uorodheshaji wa Kaya, Ajira ya Wadadisi na Mafunzo ... 6
2.6 Ukusanyaji wa Taarifa ... 6
2.7 Uchakataji wa Taarifa ... 7
2.8 Mwitiko wa Utafiti ... 7
**3 VIASHIRIA MUHIMU: UMASKINI WA KIPATO** ... 10
3.1 Mapato na Matumizi ya Kaya ... 10
3.2 Mstari wa Umasikini ... 15
3.3 Kiwango cha Umasikini wa Mahitaji ya Msingi na Chakula ... 16
3.4 Idadi ya Watu Maskini ... 18
3.5 Pengo la Umasikini ... 20
3.6 Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini ... 22
3.7 Kiwango cha Usawa ... 23
3.8 Umasikini na Muundo wa Kaya ... 24
3.8.1 Umaskini kwa Idadi ya Wanakaya ... 24

3.7.3 Umasikini na Idadi ya watoto ..... 25
3.7.4 Umaskini wa Watoto ..... 26
4.0 VIASHIRIA VYA UMASKINI VISIVYO VYA KIFEDHA ..... 29
4.1 Muundo wa Kaya ..... 30
4.1.1 Wastani wa Ukubwa wa Kaya ..... 30
4.1.2 Uwiano wa Wanakaya Tegemezi ..... 32
4.2 Hali ya Makazi ..... 33
4.3 Matumizi ya Umeme ..... 34
4.4 Matumizi ya Nishati ..... 36
4.4.1 Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kuangazia ..... 36
4.5 Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kupikia ..... 37
4.6 Vyanzo vya Maji ..... 38
4.7 Huduma ya Vyoo ..... 39
4.8 Umiliki wa Akaunti za Benki ..... 40

# Orodha ya Jadweli


Jadweli 2.1: Mapendekezo ya Mgawanyo wa Sampuli HBS 2019/20, Zanzibar .......................... 4

Jadweli 2.2: Muhtasari wa Viashiria vya Matokeo Muhimu kwa Maeneo, HBS 2014/15 na 2019/20 Zanzibar .......... 8

Jedwali 3.1: Wastani wa Matumizi ya Kaya kwa Mwezi, na Wastani wa Matumizi kwa Mtu Mzima kwa Mwezi kwa Eneo, Wilya na Aina ya Wastani ya Matumizi, 2019/20 Zanzibar HBS .......... 10

Jedwali 3.2: Wastani wa Matumizi kwa Mtu kwa Makundi ya Bidhaa na kwa Eneo (kwa Bei za Mwaka wa Utafiti, 2009/10, 2014/15 and 2019/20 Zanzibar HBSs .................... 15

Jedwali 3.3: Mstari wa Umaskiniwa Mahitaji ya Msingi na Chakula (shilingi) kwa Kipimo cha Mtu Mzima kwa mwezi 2009/10, 2014/15 and 2019/20 Zanzibar HBSs ............. 16

Jedwali 3.4 Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi kwa Wilaya, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBSs .......... 17

Jedwali 3.5: Kiwango cha Umaskini wa Chakula (Umaskini Uliokithiri) kwa Wilaya, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBSs .......... 18

Jedwali 3. 6: Kiwango cha Umaskini kwa Eneo na Wilaya, 2019/20 Zanzibar HBS ........................ 21

Jadweli 3.7: Kiwango cha Umaskini kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya na Aina ya Umaskini, 2019/20 Zanzibar HBS .......... 25

Jedwali 3.8: Kiwango cha Umaskini kwa Idadi ya Watoto chini ya miaka 5, 2019/20 Zanzibar HBS .......... 26

Table 3.9: Umaskini wa Mahitaji ya Msingi wa Watoto kwa Wilaya, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBSs .......... 27

Jedwali 4.1: Asilimia ya Kaya zilizounganishwa na Umeme kwa Jinsi na Wilaya, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS .......... 36

Jedwali 4.2: Asilimia ya Kaya kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo, Wilaya na Aina ya Chanzo Kikuu cha Kuangazia 2019/20 Zanzibar HBS .......... 37

Jedwali 4.3: Asilimia ya Kaya kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo, Wilaya na Chanzo Kikuu Cha Nishati ya Kupikia, 2019/20 Zanzibar HBS .......... 38

Jedwali 4.4: Asilimia ya kaya zenye Chanzo Kikuu cha Maji Kilichoimarishwa wakati wa Mvua na Kiangazi kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya , Eneo na Wilaya 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS .......... 39

Jedwali 4.5: Asilimia ya Kaya zenye Aina yoyote ya Choo, Zisizo na Choo kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo na Wilaya, Zanzibar 2014/15 and 2019/20 HBS .......... 40

Jedwali 4.6: Asilimia ya Kaya zenye angalau Mwanakaya mmoja mwenye Akaunti ya Benki kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo na Wilaya, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS ........ 41

## Orodha ya Michoro


Mchoro 3.1: Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 ........ 16
Mchoro 3.2: Umasikini wa Chakula (Kiwango cha Umaskini Uliokithiri) kwa Eneo, 2009/10, ... 17
Mchoro 3.3: Asilimia ya Watu Wanaoishi katika Umaskini wa Mahitaji ya Msingi kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBSs .................................................. 19
Mchoro 3.4: Asilimia ya watu wanaoishi katika Umaskini Uliokithiri (Chakula) kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBSs .................................................. 19
Mchoro 3.5: Mgawanyo wa Watu Maskini (Idadi) kwa aina ya Umaskini na Wilaya, 2019/20 Zanzibar HBS ........................................................................................ 20
Mchoro 3.6: Umaskini wa kina wa Mahitaji ya Msingi kwa eneo, Zanzibar HBS 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBSs ................................................................ 22
Mchoro 3.7: Kiwango cha Umasikini Uliokithiri (Chakula) kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 and 2019/20 Zanzibar HBSs .......................................................................... 22
Mchoro 3.8: Mwenendo wa Viashiria vya Umasikini, 2009/10 to 2019/20 Zanzibar HBSs ........ 23
Mchoro 3. 9: Fahirisi ya Gini kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBSs .......... 24
Mchoro 3. 10: Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji Msingi kwa Idadi ya Wanakaya, 2014/15 na 2019/19 HBS Zanzibar .......................................................................... 24
Mchoro 3. 11: Umasikini wa Mahitaji ya Msingi kwa Watoto (Miaka 0-17 kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBSs ................................................................ 27
Mchoro 4.1 : Wastani wa Ukubwa wa Kaya kwa Eneo, 2009/10 na 2019/20 .......................... 30
Mchoro 4.2: Wastani wa Ukubwa wa Kaya kwa Jinsi Mkuu wa Kaya....................................... 31
Mchoro 4.3: Wastani wa Ukubwa wa Kaya kwa Wilaya, 2009/10 to 2019/20 Zanzibar HBSs ... 32
Mchora 4. 4: Asilimia ya Tegemezi na Wasio Tegemezi kwa Eneo na Jinsi 2019/20 Zanzibar HBS ........................................................................................................ 32
Mchoro 4. 5: Asilimia ya Tegemezi na Wasio Tegemezi kwa Wilaya, Zanzibar 2019/20 HBS ...... 33
Mchoro 4. 6: Asilimia ya Kaya zennye Nyumba zilizojengwa kwa kutumia vifaa vya Kisasa kwa Eneo, 2019/20 Zanzibar HBS ........................................................................ 34
Mchoro 4.7: Asilimia ya Kaya zenye Nyumba zilizojengwa kwa kutumia vifaa vya Kisasa kwa Aina ya Vifaa, 2009/10 to 2019/20 Zanzibar HBSs ..................................................... 34
Mchoro 4.8: Asilimia ya Kaya zilizounganishwa na Umeme wa ZECO kwa Eneo 2009/10 hadi 2019/20 Zanzibar HBSs .......................................................................... 35
Ramani 1: Wastani wa Matumizi ya Kaya (Shilingi) kwa Mtu Mzima kwa Mwezi Kiwilaya, 2019/20 HBS ........................................................................................ 11
Ramani 2: Wastani wa Matumizi kwa (Shilingi) ya Mtu Mzima yasiyo ya Chakula kwa Mwezi Kiwilaya, 2019/20 HBS ........................................................................... 12
Ramani 3: Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi Kiwilaya, 2019/20 HBS .................. 13
Ramani 4: Wastani wa Matumizi ya (Shilingi) ya Mtu Mzima ya Chakula kwa Mwezi Kiwilaya 2019/20 HBS ........................................................................................ 14
Ramani 5: Watoto Waliochini ya Mstari wa Umaskini wa Chakula Kiwilaya,2019/20 HBS ....... 28
Ramani 6: Watoto Walio chini ya Mstari wa Umaskini wa Mahitaji ya Msingi Kiwilaya, 2019/20 HBS ........................................................................................................ 29

# DIBAJI

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) wa mwaka 2019/20 ni wa tano kufanyika katika mtiririko wa tafiti za Kitaifa za aina hii zilizofanywa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) Zanzibar. Tafiti zilizotangulia zilifanyika mwaka 2014/15, 2009/10, 2004/05 na 1992.

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kukusanya taarifa kwa ajili ya kupima mafanikio yaliyopatikana katika juhudi za Serikali za kupunguza Umaskini na katika utekelezaji wa Sera za maendeleo, programu na miradi iliyolenga kuimarisha hali za maisha za kaya. Vile Vile, itasaidia katika tathmini ya Malengo Endelevu ya Kimataifa (SDGs), kukusanya taarifa za kaya zinazohusiana na kaya binafsi juu ya shughuli za kiuchumi, mapato na matumizi ya kaya, taarifa za makazi na umiliki wa vifaa vya thamani. Utafiti wa mapato na matumizi ya kaya wa mwaka 2019/20 utatoa taarifa muhimu zitakazotumika kufanya mapitio katika kukadiria Pato la Taifa, vile vile kupata mkoba mpya wa bidhaa na wenye taarifa za sasa za matumizi zinazoitajika kwa ajili ya kufanya mapitio   Faharisi ya Bei (CPI).

Ripoti hii inatoa muhtasari wa viashiria muhimu vya umasikini na visivyo vya umasikini katika ngazi ya Taifa, Vijijini na Mijini; na katika ngazi ya wilaya za Zanzibar. Taarifa za kina zitapatikana katika ripoti kuu ya utafiti huu wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2019/20.

Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Shirika la Fedha la Dunia (WB), Shirika la Umoja wa Mataifa la kusaidia watoto (UNICEF), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP-(ZJP), Shirika la Mataifa la Wanawake (UN-WOMEN) na Benki ya Tanzania (BOT) kwa misaada ya Kifedha na Kiufundi wakati wote utekelezaji wa utafiti huu. Shukrani za pekee ziwaendee watendaji wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) kwa kusimamia vyema mchakato wote wa ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za utafiti huu.

Mwisho, napenda kuzishukuru kaya zote zilizoshiriki, ushirikianao wao ulikuwa ni muhimu katika ukusanyaji wa taarifa za utafiti wa mapato na matumizi ya kaya wa mwaka 2019/20. Shukrani nyingi pia ziende kwa Masheha kwa ushirikiano wao wakati wote wa ukusanyaji wa taarifa za utafiti huu.

Ni matumaini yangu kuwa, muhtasari wa ripoti ya utafiti huu itakuwa ni chanzo ya taarifa kwa wapanga na watunga sera, watafiti, mashirika yasiyi ya kiserikali na wadau wengine.

Mheshimiwa, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa (MHR)
**Waziri wa Fedha na Mipango,**
**Zanzibar.**

## SHUKRANI

Ripoti ya viashiria ya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ya mwaka 2019/20 inawasilisha muhtasari wa viashiria muhimu vya umasikini wa Kipato na usio wa kipato vya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) wa mwaka 2019/20.. Vile vile ripoti hii inatoa ulinganisho wa matokeo ya tafiti mbili zilizotangulia za mwaka 2014/15 na 2009/10. Mafanikio ya utekelezaji wa Utafiti wa HBS wa mwaka 2019/20 umetokana misaada ya kitaalamu na kifedha kutoka katika taasisi na watu binafsi, na napenda kutoa shukrani za dhati kwa michango.

Kwanza, napenda kutoa shukrani zangu za dhati ziende kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Shirika la Fedha la Dunia (WB), Shirika la Umoja wa Mataifa la kusaidia watoto "UNICEF", Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa "UNDP-(ZJP)", ), Shirika la Mataifa la Wanawake "UN-WOMEN" na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa misaada ya Kifedha na Kiufundi wakati wote utekelezaji wa utafiti huu. Napenda kumshkuru Mtaalamu wa ODI aliyemaliza muda wake, Bw. Nathan Price, kwa kuandaa sampuli na Ms. Sylvia Meku wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu(NBS) kwa msaada wake; Dkt. Sasun Tsirunyan, Mtaalamu wa Kimataifa wa uchambuzi wa taarifa za umaskini na Dkt. Rob Swinkels na Ms Elithabeth Ann Talbet wa Shirika la Fedha Duniani (WB) kwa misaada yao ya kiufundi. OCGS inawashukuru wote walioshiriki katika uandishi wa ripoti hii wakiwemo, Ms Khadija Khamis Hamad, Abdul Majid Jecha, Fahima Issa, Abdullah Othman, Hashim Uzia, na "ODI Fellow" Ndugu Francis Lavoe kwa michango yake ya kiufundi.

Vile Vile, OCGS inapenda kuzishukuru kaya zilizochaguliwa kwa kutoa ushirikiano na kutumia muda wao wakati na kutembelewa mara kwa mara na wadadisi kwa mahojianao wakati wote wa ukusanyaji wa taarifa za utafiti huu. Shukrani za dhati pia ziende kwa Maofisa wa Wilaya na wadadisi kwa kutoa msaada endelevu kwa kuwa makini katika ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa wanakaya. Mwisho, napenda kutambua michango ya wajumbe wa kamati ya wataalamu wakati wote wa utekelezaji wa utafiti huu.

Ripoti hii inatarajiwa kutumika katika uandaaji wa mipango katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau wengine, na pi kuibua tafiti za kina na uchambuzi wa kina wa sekta mbali mbali za uchumi. Ni matumaini yangu kwamba, ripoti hii itakuwa ni chanzo muhimu cha taarifa kwa wapanga mipango na Sera, mashirika yasiyo ya kiserikali, wanavyuo, na wadau wengine wakiwemo wa ngazi ya kitaifa, mikoa na taasisi za kimataifa.

Mayasa M. Mwinyi,
**Mtakwimu Mkuu wa Serikali,**
**Zanzibar.**

# UTANGULIZI

## 1.0 Muhtasari

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) Zanzibar imekuwa ikifanya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) tokea mwaka 1992 kwa kukusanya taarifa za matumizi, manunuzi na mapato na viashiria vingine vya kijamii na kiuchumi kwa Zanzibar. Utafiti wa mwanzo wa mapato namatumizi ya kaya ulifanyika mwaka 1992 ambao ulitoa viashiria muhimu vya kijamii na kiuchumi katika ngazi ya Taifa na ya chini ya Taifa Zanzibar.Tokea hapo OCGS ilifanikiwa kutekeleza kikamilifu tafiti nne za aina hii. Utafiti wa mwaka 2019/20 HBS umetoa taarifa sahihi kwa ajili ya Sera kutoa maamuzi, kuandaa mipango, ufuatiliaji na tathmini katika ngazi za Kimataifa, Kitaifa na wilaya za Zanzibar.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ikiwa ni pekee yenye dhamana ya kutoa takwimu rasmi, pamoja shughuli zake nyingine, ina jukumu la kufanya tafiti za Kitaifa. Hivyo, jukumu la OCGS ni kutoa taarifa za sasa kwa ajili ya tathmini ya MKUZA na programu nyingine za maendeleo nchini za kitaifa. OCGS imefanya utafiti wa mwaka 2019/20 kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya taarifa katika ngazi ya Kitaifa ya Tathmini ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020, MKUZA, mapitio ya Pato la Taifa na kwa ajili ya tathmini ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia(SDGs).

Katika utekelezaji wa utafiti huu, OCGS ilishirikia na Tume ya Mipango Zanzibar chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.  Taasisi nyingine zilizoshiriki ni Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na idara Maalum za Serikali (PORALG); Sheha; Benki Kuu ya Tanzania (BOT); Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Idara ya Lishe chini ya Wizaraya Afya, Idara Uhakika wa Chakula chini ya Wizara ya Kilimo, Benki ya Dunia (WB); Shiraka la Umoja wa Mataoifa la Wanawake “UN Women”; Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Umoja wa Mataifa la kusaidia watoto (UNICEF). Msaada wa kiufundi wakati wote wa utekelezaji wa utafiti ulitolewa na Benki ya Dunia na UNICEF. Fedha zilitolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na washirika wa Maendeleo (Benki ya Dunia, UNDP, UNICEF, na UN Women).

## 1.1 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2019/20 ni kupata taarifa za sasa za umasikini, matumizi na viashiria vingine vya kijamii na kiuchumi kwa Zanzibar. Taarifa za HBS 2019/20 HBS zitatumika katika ufuatiliaji na tathmini ya hatua zilizofikiwa katika kupunguza umaskini na utekelezaji wa sera za maendeleo. Programu ma miradi iliyolenga kuimarisha maisha bora ya kaya. Vile vile, zitatumika katika kufanya tathmini ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, MKUZA III na Ajenda ya Dunia ya 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Malengo mengine ya utafiti wa HBS wa 2019/20 ni:

- Kupitia mwenendo wa matumizi ya bidhaa na huduma kwa kaya za Zanzibar;
- Kupata taarifa zikazosaidia kufanya Mapitio ya takwimu za Pato la Taifa na Fahirisi ya Bei ya Mlaji (CPI);
- Kupata taarifa vyingine za msingi za viashiria vya kijamii na kiuchumi kwa ajili ya kutoa viashiria vya umasikini mtambuka kwa watoto (multi-dimensional povert; na
- Kupata taarifa za mgawanyo wa mapato na matumizi ya kaya.

# 2.0 UTEKELEZAJI WA UTAFITI

Maandalizi ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) wa mwaka 2019/20 yalianza Januari mwaka 2018 kwa kuanzisha kamati ya wataalamu yenye wajumbe kutoka Wizara, Idara na Wakala wa Serikali pamoja na Wadau wa Maendeleo. Kamati ya wataalamu ilikuwa na jukumu la kutoa utaalamu na msaada wa kiufundi na kifedha kwa ajili ya utekelezaji wa utafiti huu.

## 2.1 Muundo wa Sampuli

### 2.1.1 Mbinu za Utafiti

Sampuli ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2019/20 iliundwa kutoa uwakilishi wa makisio kwa ngazi ya Kitaifa, Mjini na Vijijini na katika ngazi za wilaya zote 11 ambapo mwaka 2014/15 zilikuwa wilaya 10. Sampuli ya utafiti ilichaguliwa katika hatua mbili. Hatua ya kwanza ilihusika na uchaguzi wa maeneo ya kuhesabia watu kutokana na orodha iliyoandaliwa wakati wa Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012 na yaligawiwa kwa wilaya na kwa maeneo ya mijini na vijijini. Maeneo ya kuhesabia watu yalichaguliwa kitaalamu kwa kuzingatia idadi ya kaya ya eneo la kuhesabia watu. Hatua ya pili ya sampuli ilikuwa uchaguzi wa kaya (haikujumuisha kaya za kambi za askari, mabweni, n.k.) ambazo zimechaguliwa bila upendeleo kutokana na orodha ya kaya zilizoorodheshwa siku chache kabla ya utafiti.

Jumla ya Maeneo 235 yamechaguliwa kutokana na orodha ya maeneo ya kuhesabia watu ya Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012. Maeneo ya Kuhesabia Watu yaliwekwa kwa wilaya 11 kwa kuzingatia makosa ya kisampuli inayohitajika kwa makisio ya viashiria vya umaskini kwa ngazi ya wilaya na mjini na vijijini. Usahihi unaokubalika katika kutofautisha makisio ya umasikini kwa ngazi ya Kitaifa ni chini ya asilimia 5 na ngazi ya wilaya pamoja na mjini/vijijini ni chini ya asilimia 20.

### 2.1.2 Mgawanyiko na Ukubwa wa Sampuli

Mgawanyo na ukubwa wa sampuli ulitengenezwa kwa kutumia programu maalumu (iterating Excel Solver) kwa ajili ya kupunguza ukubwa wa mgawanyiko wa sampuli pamoja na mlinganisho wa viashiria vyengine. Mara baada ya kupatikana sampuli, sampuli kubwa ilichaguliwa kwa kila eneo la kuhesabia watu ili kupata mahitaji yenye gharama ndogo kwa kila eneo. Hii ilisababisha upatikanaji wa sampuli inayofaa zaidi yenye kaya 2,820 kati ya maeneo ya kuhesabia watu 235. Maelezo ya ukubwa wa sampuli inayotumiwa na mgawanyiko wake umeonyeshwa kwenye **Jadweli 2.1**.

Jadweli 2. 1: Mapendekezo ya Mgawanyo wa Sampuli HBS 2019/20, Zanzibar

| Na. | Wilaya | Maeneo ya Kuhesabi a Watu | Idadi ya Kaya | Maeneo ya Kuhesabi a Watu Vijijini | Maeneo ya Kuhesabi a Watu Mijini | Kaya za Vijijini | Kaya za Mjini | Kaya kwa kila Eneo la Kuhesabi a Watu | RSE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kaskazini A | 25 | 300 | 23 | 2 | 276 | 24 | 12 | 19.90% |
| 2 | Kaskazini B | 19 | 228 | 18 | 1 | 216 | 12 | 12 | 19.90% |
| 3 | Kati | 18 | 216 | 17 | 1 | 204 | 12 | 12 | 19.50% |
| 4 | Kusini | 15 | 180 | 12 | 3 | 144 | 36 | 12 | 19.90% |
| 5 | Magharibi A | 36 | 432 | 12 | 24 | 144 | 288 | 12 | 19.90% |
| 6 | Magharibi B | 39 | 468 | 11 | 28 | 132 | 336 | 12 | 19.80% |
| 7 | Mjini | 29 | 348 | *N/A | 29 | *N/A | 348 | 12 | 19.20% |
| 8 | Wete | 16 | 192 | 12 | 4 | 144 | 48 | 12 | 13.30% |
| 9 | Chake | 13 | 156 | 10 | 3 | 120 | 36 | 12 | 14.00% |
| 10 | Micheweni | 11 | 132 | 10 | 1 | 120 | 12 | 12 | 10.30% |
| 11 | Mkoani | 14 | 168 | 12 | 2 | 144 | 24 | 12 | 13.30% |
| | Zanzibar | 235 | 2,820 | 137 | 98 | 1,644 | 1,176 | 12 | 4.90% |

***Angalizo: Wilaya ya Mjini haina maeneo ya vijijini**

## 2.2 Maboresho

Katika kutekeleza Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2019/20, kumefanyika mabadiliko mbali mbali ukilinagnisha na utafiti wa mwaka 2014/15. Mabadiliko haya ni kama ifuatavyo:

*Mabadiliko ya kimuundo*

*(i)* Siku za ujazaji wa kitabu cha kumbukumbu cha mapato na matumizi ya kaya zilipunguzwa kutoka siku 28 hadi 14

*(ii)* Mageresho ya bidhaa za vyakula zinazonunuliwa na kutumiwa na kaya (COICOP) yametolewa kwa kina na kuboreshwa

*(iii)* Matumizi ya vishikwambi (tablets) kwa ajili ya kukusanya taarifa wakati wa mahojiano

*Ongezeko la moduli au maswali*

*(iv)* Module ya matumizi ya muda ili kupata viashiria vya jinsia vinavyohusiana na matumizi ya muda,

*(v)* Moduli ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi,

*(vi)* Moduli ya maradhi yasiyo ambukiza,

*(vii)* Uingiaji na utokaji wa fedha au bidhaa ndani na nje ya Zanzibar,

*(viii)* Moduli ya hali ya usalama wa chakula

*(ix)* Maswali ya hali ya lishe kwa watoto chini ya miaka mitano,

*(x)* Moduli ya mifuko ya hifadhi ya jamii na

*(xi)* Vifo vya watoto chini ya miaka mitano

## 2.3 Madodoso

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2019/20 umetumia madodoso ya aina saba yaliyoingizwa kwenye kishikwambi na dodoso la kitabu cha kumbukumbu za mapato na matumizi ya mwanakaya limetumika kwenye karatasi (Fomu VI). Madodoso yalitumika kukusanyia taarifa zinazohusu hali ya maisha (walio katika shughuli za kiuchumi, ajira, mapato na matumizi, mahitaji na matumizi ya siku, n.k.), huduma (usafiri na mawasiliano, n.k.), mambo yanayohusiana na afya (pamoja na maradhi yasiyoambukiza), mambo yanayohusiana na misaada kutoka nje ya nchi, pamoja na kuangagia matumizi ya muda.

Madodoso yaliwekwa katika hali ya Fomu na kila fomu ilikuwa na moduli tofauti. Fomu zilizotumika ni kama ifuatavyo:

1. **Fomu I:** Taarifa za kidemografia, uhai wa wazazi, uraia, elimu na kujua kusoma na kuandika, afya, hali ya soko la ajira, hali ya biashara za wanakaya zisizo za kilimo, mapato ya wanakaya yasiyo na ujira, hali ya uhai na kunyonyesha, maradhi yasiyoambukiza, hali ya ulemavu na lishe kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

2. **Fomu II:** Taarifa za hali ya makaazi ya kaya, huduma za maji na usafi, usafiri na mawasiliano, matumizi ya kaya kwa kipindi kilichopita, vifaa vya kudumu, samani, vifaa na vyombo vya ukarabati wa nyumbani, mavazi na viatu, gharama za huduma za afya, usafiri na mawasiliano, manunuzi ya vyombo vya moto, vifaa vya burudani, gharama binafsi za safari za nje na gharama za matumizi mengine ya kaya kwa kipindi kilichopita.
3. **Fomu III:** Biashara na mapato binafsi; shughuli za mwanakaya zisizo za kilimo na uwekezaji kwa miezi 12 iliyopita.

4. **Fomu IV:** Taarifa za kilimo na ufugaji, bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo, usalama wa chakula, vyakula vilivyotumika, mapato binafsi yasiyo ya vibarua, ustawi wa jamii, upatikanaji wa mali za asili na mazao yanayooteshwa na kaya.

5. **Fomu V:** Kitabu cha kumbukumbu za mapato na matumizi ya kaya kwa kila siku kwa muda siku 14.
6. **Fomu VI:** Kitabu cha kumbukumbu za mapato na matumizi ya mwanakaya kwa kila siku kwa muda siku 14 kwa mwanakaya mwenye umri wa miaka mitano na zaidi.

7. **Fomu VII:** Matumizi ya muda.

8. **Fomu VIII:** Utumaji wa pesa au vitu kutoka au kwenda Zanzibar, taarifa za kidemografia za mtumaji, muda na thamani ya fedha zinazopokelewa, matumizi ya fedha zinazopokelewa, vitu vinavyopokelewa na matumizi ya kaya kwa kuhaulisha matumizi binafsi

## 2.4 Utafiti wa Majaribio

### 2.4.1 Majaribio ya Awali

Nyenzo za utafiti zilifanyiwa majaribio ili kuhakikisha kwamba mtiririko wa maswali upo sawa na wadadisiwa wanayaelewa. Kazi hii ilifanywa na timu ya watendaji wazoefu wa HBS pamoja na wadadisi ambao walipata mafunzo jinsi ya kuuliza maswali.

### 2.4.2 Majaribio

Madodoso yalijaribiwa kwa kutumia maeneo ya mjini na vijijini ambayo hayakuchaguliwa kushiriki utafiti kwa Unguja na Pemba. Majaribio yalifanyika kwa siku 14 kwa ajili ya kupata uhalisia wa utafiti. Changamoto zilizojitokeza wakati wa majaribio zilijadiliwa kwa kina na kufanyiwa marekebisho kabla ya kuanza mafunzo ya utafiti.

## 2.5 Uorodheshaji wa Kaya, Ajira ya Wadadisi na Mafunzo

Zoezi la uorodheshaji wa kaya katika maeneo 235 yaliyochaguliwa lilifanyika mwezi wa Disemba 2018. Zoezi hili lilifanyika kwa kutumia mfumo wa ‘survey solution’ na kufuatiwa na uchaguzi wa kaya zilizohusika kwenye utafiti. Jumla ya watafiti 142 kutoka wilaya 11 waliajiriwa kwa ajili ya kufanya mahojiano katika kaya zilizochaguliwa. Mafunzo ya wakufunzi yalifanyika Pemba mwishoni mwa mwezi wa Januari mwaka wa 2019. Mafunzo kwa washiriki wote (wadadisi, wasimamizi, wasimamizi wa viwango na wahariri) wa zoezi la ukusanyaji wa taarifa za utafiti yalifanyika kwa Unguja na Pemba kwa muda wa siku 21 kuanzia tarehe 6 hadi 26 Febuari 2029.

## 2.6 Ukusanyaji wa Taarifa

Kazi ya ukusanyaji wataarifa ilichukua miezi 12 mfululizo kuanzia tarehe 1 Machi 2019 hadi tarehe 28 Febuari 2020. Kazi hii ilitumia vishikwambi vilivyounganishwa na mtandao kwa ajili ya kutuma taarifa ofisini kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

## 2.7 Uchakataji wa Taarifa

Ukusanyaji wa taarifa, uhariri na uchakataji vilifanyika sambamba. Mfumo wa 'survey solution' ilitumika kuingizia taarifa na kufuatilia utendaji wa wadadisi na wasimamizi. Mlinganisho wa taarifa ulikuwa unafanyika wakati wa ukusanyaji wa taarifa.

## 2.8 Mwitiko wa Utafiti

Kati ya kaya 2,820 zilizochaguliwa, kaya 2,778 zilishiriki mahojiano na kufanya mwitiko wa utafiti huu kuwa asilimia 98.5.

### Jadweli 2. 2: Muhtasari wa Viashiria vya Matokeo Muhimu kwa Maeneo, HBS 2014/15 na 2019/20 Zanzibar

| Viashiria | 2014/15 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Vijijini | Mjini | Jumla | Vijijini | Mjini | Jumla |
| **Sifa za Wanakaya na Makaazi** | | | | | | |
| Wastani wa watu katika kaya | 5.5 | 5.6 | 5.6 | 5.3 | 5.4 | 5.3 |
| Uwiano wa wategemezi | 49.4 | 41.9 | 46.0 | 49.1 | 40.8 | 45.4 |
| Asilimia ya wakuu wa kaya wanawake | 22.5 | 23.3 | 22.8 | 22.6 | 25.2 | 23.7 |
| Asilimia za watoto wenye umri 0-4 wenye vyeti vya | 97.1 | 99.2 | 97.7 | 99.8 | 100.0 | 99.9 |
| Asilimia za watoto wenye umri 0-17 wenye vyeti vya | 95.7 | 98.9 | 97.0 | 97.4 | 99.7 | 98.3 |
| Asilimia za kaya zenye kumiliki makaazi | 89.3 | 76.5 | 83.7 | 88.3 | 72.5 | 81.6 |
| Asilimia za kaya ambazo zilizosakafiwa sakafu za kisasa | 64.8 | 95.0 | 77.9 | 72.0 | 97.3 | 82.7 |
| Asilimia za kaya ambazo zimejengwa kuta za kisasa | 62.3 | 96.5 | 77.1 | 70.5 | 98.7 | 82.3 |
| Asilimia za kaya ambazo zimejengwa kwa paa za kisasa | 75.8 | 98 | 85.4 | 85.7 | 99.1 | 91.3 |
| Wastani wa watu kwa chumba cha kulala | 2.3 | 2.1 | 2.2 | 2.3 | 2.1 | 2.2 |
| **Elimu** | | | | | | |
| Asilimia ya watu wasio na elimu rasmi (miaka 15na zaidi) | 23.8 | 7.3 | 16.3 | 16.9 | 4.7 | 10.9 |
| Asilimia ya watu waliopata elimu wenye umri wa miaka 15 na zaidi | 76.1 | 92.3 | 83.7 | 80.9 | 94.6 | 87.4 |
| Asilimia ya wanawake walio na elimu wenye umri wa miaka 15 na zaidi | 70.4 | 89.3 | 79.4 | 76.2 | 92.2 | 83.9 |
| Uandikishwaji wa watoto elimu ya awali* | 79.5 | 87.9 | 83.7 | 82.4 | 90.4 | 85.7 |
| Uandikishwaji wa watoto elimu ya msingi* | 79.6 | 88.8 | 84.2 | 78.0 | 86.8 | 81.4 |
| Uandikishwaji wa watoto elimu ya sekondari* | 34.8 | 46.2 | 40.1 | 44.3 | 61.6 | 52.1 |
| Asilimia za kaya zilizomo ndani ya kilomita 2 kufikia skuli ya msingi | 95.4 | 98.3 | 96.5 | 97.1 | 99.0 | 97.9 |
| Wastani wa muda uliotumika kutembea hadi skuli ya msingi (Dakika) | 19.8 | 18.0 | 19.1 | 14.5 | 10.1 | 12.7 |
| Wastani wa muda uliotumika kutembea hadi skuli ya sekondari (Daakika) | 19.1 | 19.6 | 19.4 | 14.9 | 13.3 | 14.0 |
| Asilimia ya wakuu wa kaya wasio na elimu rasmi | 33.1 | 10.4 | 23.3 | 23.9 | 8.1 | 17.2 |
| **Afya** | | | | | | |
| Asilimia ya watu waliopata maradhi ndani ya wiki nne zilizopita | 13.9 | 8.0 | 11.3 | 16.9 | 13.2 | 15.2 |
| Asilimia ya watu waliopata ushauri au huduma za afya kwa kipindi cha wiki 4 zilizopita | 72.5 | 75.1 | 73.9 | 69.8 | 63.8 | 67.5 |
| Wagonjwa wasioweza kulipia huduma za afya kwa kuwa | 7.6 | 11.6 | 8.6 | 1.7 | 1.5 | 1.6 |
| Asilimia za watu nwalioridhika na huduma za afya | 79.2 | 81.8 | 80.1 | 80.3 | 76.3 | 78.9 |

| Viashiria | 2014/15 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Vijijini | Mjini | Jumla | Vijijini | Mjini | Jumla |
| Asilimia ya kaya zilivyomo ndani ya kilomita 5 kufikia vituo vya afya | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 |
| **Maji na Huduma ya Choo** | | | | | | |
| Asilimia ya kaya zinazotumia maji ya kunywa yaliyohifadhiwa | 86.3 | 96.3 | 90.5 | 88.3 | 95.9 | 91.5 |
| Asilimia ya kaya zinazopata maji ya kunywa ndani ya kilomita 1 | 95.3 | 99.0 | 96.9 | 98.0 | 99.8 | 98.8 |
| Asilimia ya kaya zenye huduma za vyoo | 72.5 | 98.3 | 83.7 | 78.9 | 99.3 | 87.5 |
| **Chanzo cha Nishati** | | | | | | |
| Asilimia ya kaya zilizounganishwa kwa umeme (ZECO) | 20.3 | 75.5 | 44.2 | 32.9 | 86.3 | 55.4 |
| Asilimia ya kaya zinazotumia umeme kwa ajili kuonea | 22.2 | 76.0 | 45.5 | 32.8 | 86.3 | 55.3 |
| Asilimia za kaya zinazotumia nishati ya mafuta ya taa kwa kuonea | 71.9 | 20.8 | 49.7 | 50.8 | 8.5 | 33.0 |
| Asilimia ya kaya zinazotumia mkaa au kuni kwa ajili ya kupikia | 97.7 | 90.4 | 94.5 | 93.9 | 79.3 | 87.7 |
| Asilimia ya kaya zinazotumia gesi ya viwandani kwa | 0.1 | 2.4 | 1.7 | 2.2 | 14.0 | 7.1 |
| **Shughuli za Kiuchumi** | | | | | | |
| Asilimia ya watu wasio na ajira wenye umri wa miaka 15 na zaidi | 5.8 | 9.8 | 7.7 | 3.5 | 8.3 | 5.9 |
| Asilimia ya kaya zinazomiliki ardhi ya kilimo au kulishia mifugo | 54.6 | 11.2 | 35.8 | 47.9 | 16.4 | 34.6 |
| **Safari kwa ajili ya Biashara na Burudani** | | | | | | |
| Asilimia ya kaya waliokwenda safari na kutumia angalau usiku mmoja katika kipindi cha miezi 12 iliyopita | 38.8 | 36.4 | 37.7 | 46.3 | 48.6 | 47.3 |
| **Umasikini na Tofauti ya Kipato** | | | | | | |
| Asilimia watu walio chini ya kiwango cha mahitaji muhimu | 40.2 | 17.9 | 30.4 | 33.7 | 15.5 | 25.7 |
| Asilimia ya watu waliochini ya kiwango cha umasikini wa chakula | 15.7 | 4.5 | 10.8 | 12.7 | 4.9 | 9.3 |
| Tofauti ya kiwango cha umasikini (Gini Coefficient) | 0.27 | 0.31 | 0.3 | 0.29 | 0.31 | 0.31 |
| Asilimia ya watoto (0-17) waliochini ya kiwango cha mahitaji muhimu | 44.8 | 19.9 | 34.7 | 38.7 | 17.3 | 30.1 |
| Asilimia ya watoto (0-17) waliochini ya kiwango cha umasikir chakula | 18.1 | 5.0 | 12.8 | 15.3 | 5.4 | 11.4 |

* Utekelezaji wa Sera ya Elimu ya mwaka 2006 imeathiri mfumo wa elimu kutoka miaka 7 ya shule za msingi na kuanza darasa la kwanza kwa miaka 7 hadi miaka 6 ya shule za msingi na kuanza darasa la kwanza miaka 6 mwaka 2016.

Mfumo wa elimu rasmi uwe 2-6-4-2-3+ (miaka 2 ya elimu ya awali, miaka 6 ya elimu ya msingi, miaka 4 ya elimu ya sekondari, miaka 2 ya kidato cha 5 na 6 na miaka 3 ya elimu ya juu)

# 3 VIASHIRIA MUHIMU: UMASKINI WA KIPATO

## 3.1 Mapato na Matumizi ya Kaya


Utafiti wa 2019/20 HBS Zanzibar, unaonesha kuwa wastani wa matumizi kwa kaya kwa mwezi in TZS 499,793. Wastani wa matumizi ni makubwa katika maeneo ya Mjini (TZS 590,491) ukiliganisha na Maeneo ya Vijijini (TZS 427,977). Kuna tofauti kubwa ya matumizi katika Wilaya kwa mwezi ambapo Wilaya ya Maghari B (TZS 656,285) inaongoza kwa wastani mkubwa wa matumizi na wilaya ya Micheweni (TZS 367,995) inawastani mdogo wa matumizi kwa mwezi.

Wastani wa matumizi kwa kipimo cha mtu mzima ipo juu katika Maeneo ya Mijini (TZS 131,212) ikilinganishwa na Kijijini (TZS 94,257), licha ya maeneo ya Vijijini kuwa na wastani wa chini ukilinganisha na mijini bado wanaoishi vijijini wapo juu wa wastani kwa kipimo cha mtu mzima **(Jadweli 3.1)**.


**Jedwali 3. 1: Wastani wa Matumizi ya Kaya kwa Mwezi, na Wastani wa Matumizi kwa Mtu Mzima kwa Mwezi kwa Eneo, Wilya na Aina ya Wastani ya Matumizi, 2019/20 Zanzibar HBS**

| Characteristics | Wastani wa Matumizi ya Kaya kwa Mwezi (shilingi) | Wastani wa Matumizi (Shilingi) ya Mtu Mzima kwa Mwezi kwa Aina Maskini | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Chakula | Zisizo cha Chakula | Jumla |
| **Eneo** | | | | |
| Vijijini | 427,977 | 59,376 | 34,881 | 94,257 |
| Mijini | 590,491 | 57,370 | 73,842 | 131,212 |
| **Wilaya** | | | | |
| Kaskazini A | 413,354 | 66,370 | 36,799 | 103,169 |
| Kaskazini B | 404,117 | 64,382 | 33,755 | 98,137 |
| Kati | 412,262 | 61,662 | 44,562 | 106,224 |
| Kusini | 390,727 | 66,353 | 46,269 | 112,622 |
| Mjini | 532,512 | 46,861 | 76,336 | 123,196 |
| Magharibi A | 596,808 | 62,825 | 63,242 | 126,067 |
| Magharibi B | 656,285 | 64,435 | 84,264 | 148,699 |
| Wete | 416,015 | 57,694 | 23,800 | 81,494 |
| Micheweni | 367,995 | 57,364 | 23,766 | 81,131 |
| Chake Chake | 517,372 | 49,873 | 44,852 | 94,725 |
| Mkoani | 458,409 | 58,411 | 28,083 | 86,494 |
| **Jumla (Wastani)** | **499,793** | **58,490** | **52,098** | **110,588** |


Ramani 1: Wastani wa Matumizi ya Kaya (Shilingi) kwa Mtu Mzima kwa Mwezi Kiwilaya, 2019/20 HBS




Ramani 2: Wastani wa Matumizi kwa (Shilingi) ya Mtu Mzima yasiyo ya Chakula kwa Mwezi Kiwilaya, 2019/20 HBS



Ramani 3: Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi Kiwilaya, 2019/20 HBS



Ramani 4: Wastani wa Matumizi ya (Shilingi) ya Mtu Mzima ya Chakula kwa Mwezi Kiwilaya 2019/20 HBS




**Jedwali Namba 3.2** inaonesha wastani kwa matumizi kwa mtu kwa aina ya bidhaa. Biadhaa zimegawika katika makundi kama yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa (*UN_ System of Classification of Individual Consumption by Purpose 'COICOP'*). Matokeo yanaonesha kuwa katika kipindi cha Miaka 10 iliyopita, matumizi ya chakula

yanaonekana kushuka kutoka asilimia 52.1 mwaka 2009/10 hadi kufikia asilimia 41.4 mwaka 2019/20 ambapo mchango wa matumizi ya vitu mbali mbali visivyo vya chakula (usafiri, mawasiliano n.k.) umeongezeka.

**Jedwali 3.2: Wastani wa Matumizi kwa Mtu kwa Makundi ya Bidhaa na kwa Eneo (kwa Bei za Mwaka wa Utafiti), 2009/10, 2014/15 and 2019/20 Zanzibar HBS**

| COICOP Category | 2009/10 | | | 2014/15 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Vijijini | Mijini | Jumla | Vijijini | Mijini | Jumla | Vijijini | Mijini | Jumla |
| Chakula na Vinywaji visivyo na Kilevi | 59.7 | 45.7 | 52.1 | 50.7 | 41.8 | 46 | 51.1 | 33.3 | 41.4 |
| Vinywaji Vyenye Kilevi na Bidhaa zaTumbaku | 0.4 | 0.2 | 0.3 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.2 | 0.2 |
| Mavazi ya Nguo na Viatu | 6.5 | 10.8 | 8.9 | 5.7 | 8.5 | 7.1 | 5.8 | 7.2 | 6.6 |
| Nyumba, Maji na Nishati | 16.8 | 19.2 | 18 | 19.2 | 18.6 | 18.9 | 21.7 | 27.2 | 24.7 |
| Samani, Vifaa vya Nyumbani na Matengenezo ya Nyumba | 4.4 | 4.8 | 4.6 | 5.8 | 5.5 | 5.6 | 4.7 | 4.8 | 4.7 |
| Afya | 1.3 | 2.0 | 1.6 | 1.7 | 1.2 | 1.4 | 1.3 | 1.3 | 1.3 |
| Usafiri | 4.0 | 6.4 | 5.3 | 5.2 | 9.3 | 7.3 | 5.8 | 9.7 | 7.9 |
| Mawasiliano | 2.0 | 3.2 | 2.6 | 3.9 | 5.0 | 4.4 | 2.4 | 3.6 | 3.0 |
| Utamaduni na Burudani | 0.3 | 0.7 | 0.5 | 1.3 | 2.9 | 2.1 | 1.4 | 2.7 | 2.1 |
| Elimu | 1.4 | 2.6 | 2.0 | 0.5 | 0.8 | 0.6 | 0.9 | 2.4 | 1.7 |
| Hoteli na Mikahawa | 1.1 | 1.5 | 1.3 | 2.6 | 2.8 | 2.7 | 1.9 | 3.2 | 2.6 |
| Bidhaa na Huduma Nyenginezo | 2.2 | 3.2 | 2.8 | 3.5 | 3.7 | 3.6 | 2.9 | 4.5 | 3.7 |
| **Jumla ya Asilimia** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** |

## 3.2 Mstari wa Umasikini

Mbinu ya kupima mahitaji ya msingi imetumika katika kupima kiwango cha Umaskini kwa Zanzibar. Mahitaji ya Msingi ni kiwango cha chini kabisa cha kipato anachohitaji mtu kwa ajili ya kukidhi mahitaji mbali mbali ya msingi ikiwemo bidha na huduma. Mahitaji ya Msingi hupimwa kwa mstari wa Umaskini ambao hujulikana kuwa ni kiwango cha chini cha mahitaji ya msingi kinachohitajika kukidhi mahitaji.

Kiwango cha Umaskini wa chakula ni gharama ya matumizi yote ya kaya ambayo yapo chini ya gharama wanayohitaji ili kukidhi mahitaji yao ya chakula. Kiwango hiki pia hujulikana kama kiwango cha umasikini ulio kithiri. Watu ambao wako chini ya kiwango hiki wanajulikana kama masikini wa kupindukia.

Mistari wa umasikini wa chakula na mahitaji ya msingi kwa utafiti wa mwaka 2019/20 ni (shilingi 47,541) na (shilingi 66,313) kwa kipimo cha mtu mzima kwa mwezi. Mistari wa umasikini kwa chakula na mahitaji ya msingi imeongezeka toka shiling 38,071 na shiling 53,377 kwa mwaka 2014/15 na kufikia shilingi 47,541 and shiling 66,318 in 2019/20 kwa mpangilio **(Jedwali 3.3)**.


**Jedwali 3. 3: Mstari wa Umaskiniwa Mahitaji ya Msingi na Chakula (shilingi) kwa Kipimo cha Mtu Mzima kwa mwezi 2009/10, 2014/15 and 2019/20 Zanzibar HBS**

| Mwaka | Mstari wa Umaskini wa Mahitaji ya Msingi (TZS kwa Mwezi) | Mstari wa Umaskiniwa chakula (Tzs kwa mwezi) |
|---|---|---|
| 2009/10 | 34,861 | 25,364 |
| 2014/15 | 53,377 | 38,071 |
| 2019/20 | 66,313 | 47,541 |


## 3.3 Kiwango cha Umasikini wa Mahitaji ya Msingi na Chakula

Kwa kutumia mistari ya umasikini, utafiti wa 2019/20 unaonesha kushuka kwa mahitaji ya msingi na chakula hadi kufikia asilimia 25.7 na asilimia 9.3 kwa Zanzibar. Matokeo pia yameonesha kuwa kuna tofauti kubwa ya kiwango cha umasikini kati ya mijini na vijijini. Umaskini wa mahitaji ya msingi umeshuka kwa asilimia 9.2 kwa kipingi cha miaka 10 iliyopita (2009/10 hadi 2019/20), hii inamaanisha kuwa kwa kila mwaka umasikini wa mahitaji ya msingi unapungua kwa asilimia moja kwa mwaka. (Mchoro 3.1 na 3.2).

**Mchoro 3.1: Kiwango cha Umasikini wa Mahitaji ya Msingi kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS**



Mchoro 3.2: Umasikini wa Chakula (Kiwango cha Umaskini Uliokithiri) kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS




Kwa ujumla mafanikio zaidi ya kupungua hali ya umaskini yanaonekana zaidi kwa wilaya ziliopo Pemba hasa katika wilaya ya Micheweni, kwani umaskini wa mahitaji ya msingi umeshuka kwa asilimia 21 toka mwaka 2014/15 hadi 2019/20 na Chake Chake umeshuka kwa asilimia 14.3 kwa kipindi hicho hicho. Kwa ujumla mafanikio ya kushuka kwa umaskini wa mahitaji ya msingi na chakula yanaonekana kushuka zadi katika wilaya za Pemba (**Jedwali 3.4 na Jedwali 3.5**)

**Jedwali 3.4 Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi kwa Wilaya, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS**

| | Umaskini wa Mahitaji ya Msingi | | | Mgawanyo wa Umaskini | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wilaya | 2014/15 | 2019/20 | Tofauti | 2014/15 | 2019/20 | Tofauti |
| Kaskazini A | 20.0 | 21.9 | 1.9 | 6.2 | 6.7 | 0.5 |
| Kaskazini B | 23.3 | 27.2 | 3.9 | 4.1 | 6.5 | 2.4 |
| Kati | 25.1 | 21.5 | -3.6 | 5.1 | 4.6 | -0.5 |
| Kusini | 26.3 | 14.8 | -11.5 | 2.4 | 1.7 | -0.7 |
| Magharibi | 14.6 | | -14.6 | 14.2 | | -14.2 |
| Magharibi A | | 14.7 | 14.7 | | 6.9 | 6.9 |
| Magharibi B | | 9.5 | 9.5 | | 5.7 | 5.7 |
| Mjini | 19.2 | 17.9 | -1.3 | 8.9 | 11.7 | 2.8 |
| Wete | 47.7 | 42.5 | -5.2 | 12.9 | 14.6 | 1.7 |
| Micheweni | 69.0 | 48.1 | -20.9 | 19.3 | 16.0 | -3.3 |
| Chake Chake | 51.6 | 37.3 | -14.3 | 13.0 | 11.7 | -1.3 |
| Mkoani | 52.4 | 44.4 | -8.0 | 14.0 | 13.9 | -0.1 |
| **Jumla** | **30.4** | **25.7** | **-4.7** | **100.0** | **100.0** | **0.0** |


**Jedwali 3.5: Kiwango cha Umaskini wa Chakula (Umaskini Uliokithiri) kwa Wilaya, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS**

| Wilaya | Umaskini wa Chakula | | | Mgawanyo wa Umaskini | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2014/15 | 2019/20 | Tofauti | 2014/15 | 2019/20 | Tofauti |
| Kaskazini A | 4.4 | 5.1 | 0.7 | 3.8 | 4.3 | 0.5 |
| Kaskazini B | 7.0 | 7.0 | 0.0 | 3.5 | 4.6 | 1.1 |
| Kati | 7.2 | 6.0 | -1.2 | 4.1 | 3.5 | -0.6 |
| Kusini | 6.0 | 1.7 | -4.3 | 1.6 | 0.5 | -1.1 |
| Magharibi | 3.5 | | -3.5 | 9.7 | | -9.7 |
| Magharibi A | | 5.1 | 5.1 | | 6.6 | 6.6 |
| Magharibi B | | 2.0 | 2.0 | | 3.3 | 3.3 |
| Mjini | 5.0 | 5.7 | 0.7 | 6.5 | 10.4 | 3.9 |
| Wete | 15.7 | 17.1 | 1.4 | 11.9 | 16.3 | 4.4 |
| Micheweni | 32.6 | 18.7 | -13.9 | 25.8 | 17.2 | -8.6 |
| Chake Chake | 24.4 | 19 | -5.4 | 17.3 | 16.5 | -0.8 |
| Mkoani | 21.0 | 19.4 | -1.6 | 15.8 | 16.8 | 1.0 |
| **Jumla** | **10.8** | **9.3** | **-1.5** | **100** | **100** | **0** |


## 3.4 Idadi ya Watu Maskini

Utafiti wa mwaka 2019/20 HBS, karibu roba tatu (asilimia 73.3) ya watu wanaoishi katika umasikini wa mahitaji ya msingi wanaishi vijijini. Watu wenye umasikili uliokithiria wana munekano sawa **(Mchoro 3.3 and Mchoro 3.4)**. Wilaya ya Micheweni ina idadi kubwa ya watu masikini wa mahitaji ya msingi na umasikini uliokithiri na wilaya ya Kusini ina idadi ndogo ya watu wenye umaskini wa kipato na uliokithiri **(Mchoro 3.5)**.


Mchoro 3.3: Asilimia ya Watu Wanaoishi katika Umaskini wa Mahitaji ya Msingi kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS





Mchoro 3.4: Asilimia ya watu wanaoishi katika Umaskini Uliokithiri (Chakula) kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS



Mchoro 3.5: Mgawanyo wa Watu Maskini (Idadi) kwa aina ya Umaskini na Wilaya, 2019/20




Jumla ya watu masikini 417,256




Jumla ya Watu wenye Umaskini wa Chakula 150,840

## 3.5 Pengo la Umasikini

Pengo la umasikini ni wastani wa upungufu wa matumizi yote ya mahitaji ya msingi kwa kipimo cha mtu mzima, yanayowezesha kuwatoa watu wenye umasikini ili wafikie mstari wa kupima kiwango cha umasikini. Kipimo hiki kinawezesha kutambua kina cha umasikini

Jedwali **3.5** inaonesha kwamba pengo la Umaskini (Umaskini wa mahitaji ya Msingi) kwa Zanzibar kwa utafiti wa 2019/20 HBS ni asilimia 5.8, pengo la umaskini liko juu vijijini (asilimia 8.1) ukilinganisha na Mijini (asilimia 3.0). Hii inamanisha kuwa watu wa vijijini wamezama katika umaskini zaidi kulinganisha na mijini. Ukilinganisha na wilaya zote Wilaya ya Micheweni watu wake wengi wapo katika dimbwi la umaskini wa mahitaji ya msingi (asilimia 12) na Magharibi B ina aslimia ndogo kuliko zote (asilimia 1.7).


Mwenendo wa umasikini wa pengo la mahitaji ya msingi Zanzibar yanaonesha kushuka kwa kasi katika kipindi cha mwongo mmoja (miaka 10) kutoka asilimia 8.2 mwaka 2009/10 hadi kufikia asilimia 5.8 mwaka 2019/20 HBS. Mwenendo sawa wa kushuka pia umeonekana katika umasikini uliokithiri (umasikini wa chakula) kwa kipindi hicho hicho kama inayoonekana (**Mchoro 3.6**).

Kitu muhimu zaidi, katika kupima Fahirisi ya Pengo la umaskini ni kujua kiwango gani cha fedha kinahitajika ilikuwatowa watu katika wimbi la umaskini Zanzibar. Kiasi cha fedha hicho ni kuchukua pengo la umaskini (0.058) kwa kuzidisha na jumla ya idadi ya watu wanaoishi katika kaya binafsi (1,625,589) kiwango cha mstari wa umaskini kwa mahitaji ya msingi (shilingi 66,313) kwa mwaka 2019/20. Kiasi cha shilingi ya Tanzania 6,252,265,635 kwa mwezi (sawa na dola ya Kimarekani 2.7 kwa mwezi) zinahitajika kuondoa/kuwaweka juu ya mstari ya umaskini wa mahitaji ya msingi kwa watu walio chini ya mstari wa umaskini Zanzibar.


**Jedwali 3. 6: Kiwango cha Umaskini kwa Eneo na Wilaya, 2019/20 Zanzibar HBS**

| Kipengele | Umaskini wa Mahitaji ya Msingi | | | Umaskini wa Chakula | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiwango | Kina | Kina kwa kuzingatia tofauti ya kipato | Kiwango | Kina | Kina kwa kuzingatia tofauti ya kipato |
| **Eneo** | | | | | | |
| Vijijini | 33.7 | 8.1 | 2.8 | 12.7 | 2.3 | 0.6 |
| Mijini | 15.5 | 3.0 | 0.9 | 4.9 | 0.7 | 0.2 |
| **Wilaya** | | | | | | |
| Kaskazini A | 21.9 | 3.9 | 1.0 | 5.1 | 0.4 | 0.1 |
| Kaskazini B | 27.2 | 5.9 | 1.9 | 7.0 | 1.3 | 0.4 |
| Kati | 21.5 | 4.3 | 1.4 | 6.0 | 1.4 | 0.3 |
| Kusini | 14.8 | 1.8 | 0.3 | 1.7 | 0.0 | 0.0 |
| Mjini | 17.9 | 3.1 | 0.9 | 5.7 | 0.6 | 0.1 |
| Magharibi A | 14.7 | 3,0 | 0.9 | 5.1 | 0.7 | 0.2 |
| Magharibi B | 9.5 | 1.7 | 0.5 | 2.0 | 0.4 | 0.1 |
| Wete | 42.5 | 10.3 | 3.7 | 17.1 | 3.2 | 0.9 |
| Micheweni | 48.1 | 12.0 | 4.3 | 18.7 | 3.5 | 1.1 |
| Chake Chake | 37.3 | 11.0 | 4.0 | 19 | 3.3 | 0.9 |
| Mkoani | 44.4 | 11.6 | 4.2 | 19.4 | 3.7 | 1.0 |
| **Jumla (wastani)** | **25.7** | **5.8** | **2** | **9.3** | **1.6** | **0.4** |

Mchoro 3.6: Umaskini wa kina wa Mahitaji ya Msingi kwa eneo, Zanzibar HBS 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS





Mchoro 3.7: Kiwango cha Umasikini Uliokithiri (Chakula) kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 and 2019/20 Zanzibar HBS




## 3.6 Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini

Umasikini wa mahitaji ya msingi umepungua kutoka asilimia 34.9 mwaka 2009/10 HBS hadi asilimia 25.7 mwaka 2019/20 HBS. Vile vile, umaskini wa chakula ulipungua kutoka asilimia 11.7 mwaka 2009/10 HBS hadi kufikia asilimia 9.3 mwaka 2019/20 HBS (**Mchoro 3.8**).


Mchoro 3.8: Mwenendo wa Viashiria vya Umasikini, 2009/10 to 2019/20 Zanzibar HBS




## 3.7 Kiwango cha Usawa

Tofauti ya kipato ni jinsi gani ambavyo mgawanyo wa kipato hauko sawa baina ya kaya katika jamii, matumizi kwa kipimo cha mtu mzima hutumika kupima usawa kipato katika jamii, hujulikana maka faharisi ya "Gini". Faharisi ya jini huanza kupima 0 (Matumizi sawa) 1pia (huchukuliwa kama mtu mmoja ana matumizi ya nchi nzima). Matokeo ya mwaka 2019/20 HBS yanaonesha Faharisi ya Gini ni 0.31, Faharisi ya Gini inabaki kuwa sawa kwa tafiti zilizopita za HBS 2009/10 na 2014/15. Faharisi ya Gini inaonesha kuwa watu wanaoishi Mijini kuna usawa zaidi ikilinganishwa vijijini. **(Mchoro 3.9)**.

Mchoro 3. 9: Fahirisi ya Gini kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBSs





## 3.8 Umasikini na Muundo wa Kaya

### 3.8.1 Umaskini kwa Idadi ya Wanakaya

Kuna uhusiano mkubwa kati ya kiwango cha umaskini na idadi kaya. Kiwango cha umaskini kinaonekana kuongezeka kadiri ya idadi ya watu wanavyoongezeka katika kaya. Kutoka kwa matokeo ya 2019/20, karibu nusu (asilimia 46.3) ya mahitaji ya kimsingi watu masikini wanaishi katika kaya zilizo na washiriki 10 au zaidi. Hii inawakilisha kupungua kutoka asilimia 56.4 mnamo 2014/15 (Mchoro 3.10).

Mchoro 3. 10: Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji Msingi kwa Idadi ya Wanakaya, 2014/15 na 2019/19 HBS Zanzibar



### 3.8.2 Umasikini kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya

Matokeo ya Utafiti wa 2019/20HBS yanaonyesha hali ya umaskini wa mahitaji ya msingi na chakula (umaskini uliokithiri) yanaonekana Zaidi katika kaya zinazoongozwa na wanake ukilinganisha na wanaume. Jedwali 3.11; hali ya umaskini wa mahitaji ya msingi ni asilimia 30 kwa kaya zinazoongozwa na wanawake na asilimia 24.4 ya kaya zinazoongozwa na wanaume. Kwa upande mwengine umasikini wa chakula kwa kaya zinazoongozwa na wanawake ni asilimia 11.3 ambayo ni kubwa ukilinganisha na kaya zinazoongozwa na wanaume Asilimia 8.7) (Jadweli 3.7).

**Jadweli 3. 7: Kiwango cha Umaskini kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya na Aina ya Umaskini, 2019/20 Zanzibar HBS**

| Jinsi ya Mkuu wa kaya | Umaskini wa Mahitaji ya Msingi | | | Umaskini wa Chakula | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiwango | Kina | Kina kwa kuzingatia tofauti ya kipato | Kiwango | Kina | Kina kwa kuzingatia tofauti ya kipato |
| Mwanaume | 24.4 | 5.5 | 1.8 | 8.7 | 1.4 | 0.4 |
| Mwamke | 30 | 7.1 | 2.6 | 11.3 | 2.3 | 0.7 |

### 3.8.3 Umasikini na Idadi ya watoto

Matokeo ya HBS 2019/20 yanaonesha umaskini unatofautiana kutokana na idadi ya watoto walio chini ya miaka 5 katika kaya. **Jadweli 3.8** inaonesha kuwa kuna uhusiano baina ya idadi ya Watoto chini ya miaka 5 na umaskini, Kiwango cha umasikini wa mahitaji maalumu katika kaya zisizo na watoto chini ya miaka 5 ni asilimia 19.9), kadri ya idadi ya watoto wanavyoongezeka ndio hali ya umaskini wa mahitaji ya msingi invyo ongezeka. Hakuna toufauti baina ya umaskini wa mahitaji ya msingi na umaskini wa chakula na idadi ya watoto chini ya miaka 5, kwani umasikini wa chakula unaongezeka toka asilimia 7.2 kwa kaya zisizo na watoto hadi kufikia asilimia 40.8 kwa kaya zenye watoto 6 au zaidi.

**Jedwali 3. 8: Kiwango cha Umaskini kwa Idadi ya Watoto chini ya miaka 5, 2019/20 Zanzibar HBS**

| Idadi ya Watoto chini ya Umri wa miaka 5 | Umaskini wa Mahitaji ya Msingi | | | Umaskini wa Chakula | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiwango | Kina | Kina kwa kuzingatia tofauti ya kipato | Kiwango | Kina | Kina kwa kuzingatia tofauti ya kipato |
| Hakuna mtoto | 19.9 | 4.5 | 1.5 | 7.2 | 1.2 | 0.4 |
| Mtoto 1 | 21.9 | 4.5 | 1.4 | 6.4 | 1.1 | 0.3 |
| Watoto 2 | 27.5 | 6.3 | 2.2 | 9.6 | 1.9 | 0.6 |
| Watoto 3-5 | 42.7 | 10.9 | 3.8 | 19.6 | 3.1 | 0.7 |
| Watoto 6 au zaidi | 100.0 | 13.0 | 3.9 | 40.8 | 1.5 | 0.1 |

### 3.7.4 Umaskini wa Watoto

Matokeo ya HBS 2019/20 yanaonesha kuwa mtoto mmoja ya watatu (asilimia 30.1) ya watoto wote wenye umri 0 hadi 17 wapo katika umaskini wa mahitaji ya msingi. Kwa kipindi cha mwongo mmoja (Miaka 10) iliyopita umaskini wa watoto umepungua kwa asilimia 10 kutoka asilima 39.7 mwaka 2009/10 HBS hadi kufikia asilimia 30.1 kwa mwaka 2019/20 HBS, hii inamaaniasha kwa umskini umeshuka takriban kwa asilimia moja kila mwaka.

Watoto wanaoishi katika maeneo ya vijijini wengi wao wamo katika kaya zenye umaskini wa mahitaji ya msingi kulinganisha na wanaoishi Mijini. Uwiano ya watoto wanaoishi katika umaskini wa mahitaji ya msingi kwa vijijini umepungua (aslimia 6.1) ukilinganisha na maeneo ya mjini (aslimia 2.6) kwa kipindi cha miaka 5. Umasikini wa watoto katika maeneo ya mjini umepungua kwa asilimia 15 kwa mwongo mmoja uliopita na maeneo ya vijijini kwa karibu asilimia 6 (Mchoro 3.11).

Katika ngazi ya wilaya umasikini wa mahitaji ya msingi kwa watoto umepungua zaidi katika wilaya za Pemba hasa kwa wilaya ya Micheweni toka asilimia 72.1 kwa mwaka 2014/15 hadi kufikia aslimia 52.4 mwaka 2019/20 Wilaya nyengine zilizopiga hatua muhimu ni  Chakechake, Mkoani na Kusini na Kati (**Jedwali 3.9**).

Mchoro 3. 11: Umasikini wa Mahitaji ya Msingi kwa Watoto (Miaka 0-17 kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS







Table 3. 9: Umaskini wa Mahitaji ya Msingi wa Watoto kwa Wilaya, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS

| | Watoto Walio chini ya Mstari wa Umaskini wa Mahitaji ya Msingi | | | Watoto Waliochini ya Mstari wa Umaskini wa Chakula | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wilaya | 2009/10 | 2014/15 | 2019/20 | 2009/10 | 2014/15 | 2019/20 |
| Kaskazini A | 32.3 | 23.5 | 24.1 | 5.3 | 5.4 | 5.3 |
| Kaskazini B | 30.9 | 25.5 | 29.9 | 8.3 | 8.3 | 7.2 |
| Kati | 29.3 | 29.7 | 24 | 8.1 | 8.3 | 7.4 |
| Kusini | 25.6 | 26.7 | 18.2 | 4.5 | 5.5 | 1.9 |
| Magharibi | 29 | 16.1 | | 7.4 | 3.6 | |
| Magharibi A | | | 15.8 | | | 5.7 |
| Magharibi B | | | 12.1 | | | 2.3 |
| Mjini | 29.8 | 21.7 | 19.9 | 6.2 | 5.3 | 6.4 |
| Wete | 53.7 | 51.6 | 47.7 | 22.7 | 18 | 19.1 |
| Micheweni | 61.2 | 72.1 | 52.4 | 21.4 | 35.2 | 22.3 |
| Chake Chake | 43.7 | 56.4 | 42.4 | 23.9 | 28.1 | 23.5 |
| Mkoani | 52.5 | 57.2 | 47.9 | 23.7 | 24 | 20.8 |
| **Jumla (Wastani)** | **39.7** | **34.7** | **30.1** | **13.7** | **12.8** | **11.4** |

Ramani 5: Watoto Waliochini ya Mstari wa Umaskini wa Chakula Kiwilaya,2019/20 HBS



Ramani 6: Watoto Walio chini ya Mstari wa Umaskini wa Mahitaji ya Msingi Kiwilaya, 2019/20 HBS




# 4.0 VIASHIRIA VYA UMASKINI VISIVYO VYA KIFEDHA

## 4.1 Muundo wa Kaya

### 4.1.1 Wastani wa Ukubwa wa Kaya


Wastani wa ukubwa wa kaya unapatikana kwa kuchukua idadi ya watu wanaoishi katika kaya binafsi na kugawanya na idadi ya kaya binafsi. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa wastani wa kaya Zanzibar ni watu 5.3, maeneo ya mijini yalikuwa na wastani mkubwa wa kaya (watu 5.4) ikilinganishwa na maeneo ya vijijni (watu 5.3). Matokeo yameonesha kupungua kidogo kwa wastani wa ukubwa wa kaya kutoka watu 5.6 mwaka 2014/15 hadi watu 5.3 mwaka 2019/20. Mwendendo katika maeneo ya mijini unaonesha kupungua kwa wastani wa ukubwa wa kaya kutoka watu 5.7 mwaka 2009/10 hadi watu 5.4 mwaka 2019/20 **(Mchoro 4.1)**.

**Mchoro 4.1: Wastani wa Ukubwa wa Kaya kwa Eneo, 2009/10, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS**




Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa, kaya zinazoongozwa na wanaume zina wastani mkubwa zaidi wa ukubwa wa kaya ikilinganishwa na kaya zinazoongozwa na wanawake (Mchoro 4.2). Ukubwa wa Kaya unatofautiana kwa wilaya. Wilaya za Pemba zina kaya kuwa zikilinganishwa na kaya za Unguja. Kwa mfano, Wilaya ya Chake Chake ina wastani mkubwa wa kaya (watu 6.5) ambapo wilaya ya Kusini ina wastani mdogo wa kaya (watu 4.1) kama inavyoonesha katika **Mchoro 4.2**. Mpangilio huo umeonekana pia katika tafiti za 2009/10 and 2014/15 (**Mchoro 4.3**).

**Mchoro 4.2: Wastani wa Ukubwa wa Kaya kwa Jinsi Mkuu wa Kaya 2019/20 Zanzibar HBS**




**Mchoro 4.3: Wastani wa Ukubwa wa Kaya kwa Wilaya, 2009/10 to 2019/20 Zanzibar HBSs**




## 4.1.2 Uwiano wa Wanakaya Tegemezi

Uwiano wa wanakaya tegemezi unapatikana kwa kuchukua watu wenye umri wa chini ya miaka 15 na wale wenye umri wa miaka 65 na zaidi na kugawanya na idadi ya watu. Matokeo yameonesha kuwa wastani wa watu tegemezi ni asilimia 45.4. Maeneo ya Vijijini yana idadi kubwa ya watu tegemezi (asilimia 49.1 ikilinganishwa na maeneo ya mijini (asilimia 40.8). Wanaume tegemezi ni wengi (asilimia 46.3) ikilinganishwa na wanawake tegemezi (asilimia 44.6) **Mchoro 4.4.**


**Mchora 4. 4: Asilimia ya Tegemezi na Wasio Tegemezi kwa Eneo na Jinsi 2019/20 Zanzibar HBS**




Uwiano wa wanakaya tegemezi unatofautiana kati ya wilaya. Kwa mfano, wilaya ya Mkoani ina uwiano mkubwa wa wanakaya tegemezi (asilimia 55), ikifuatiwa

wilaya nyingine za Pemba na wilaya ya Mjini ina uwiano mdogo wa wanakaya tegemezi (asilimia 38.3) **(Mchoro 4.5).**

**Mchoro 4. 5: Asilimia ya Tegemezi na Wasio Tegemezi kwa Wilaya, Zanzibar 2019/20 HBS**





## 4.2 Hali ya Makazi


Kiwango cha Kaya zinazotumia vifaa vya kisasa kwa kujengea kimeimarika zaidi katika kipindi cha miaka 10 iliyopita **(Mchoro 4.7)**. Matokeo ya utafiti wa HBS wa mwaka 2019/20 yameonesha kuwa asilimia 82.3 ya kaya wana sakafu za kisasa (zege au saruji, vigae au mbao); Asilimia 82.7 wana kuta imara zilizojengewa kwa (Matofali ya kuchoma, zege, saruji au mawe), na asilimia 91.1 ya kaya zimeezekwa kwa vifaa vya kisasa (bati, zege, na vigae. Kaya za mijini zina asilimia kubwa ya nyumba zilizotumia vifaa vya kisasa kwa kuezekea, kuta na kusakafia ikilinganishwa na kaya za vijijini (**Mchoro 4.7).**



Mchoro 4. 6: Asilimia ya Kaya zennye Nyumba zilizojengwa kwa kutumia vifaa vya Kisasa kwa Eneo, 2019/20 Zanzibar HBS





Mchoro 4.7: Asilimia ya Kaya zenye Nyumba zilizojengwa kwa kutumia vifaa vya Kisasa kwa Aina ya Vifaa, 2009/10 to 2019/20 Zanzibar HBS




## 4.3 Matumizi ya Umeme

Matokeo yaliyomo kwenye **Mchoro 4.8** yanaonesha kuwa, kuwa mabadiliko makubwa ya kaya zilizounganishwa na umeme katika kipindi cha miaka 10 iliyopita kutoka asilimia 38.3 mwaka 2009/10 hadi asilimia 55.4 mwaka 2019/20. Matokeo yameonesha tofauti kati ya kaya ziliunganishwa umeme kwa mijini na vijijini. Katika maeneo ya vijijini kuna takriban kaya Tatu (3) kwa kila kaya 10 (asilimia 32.9) wakati katika maeneo ya mijini karibu kaya Tisa (9) kwa kila kaya 10(asilimia 86.3) zimeunganishwa na umeme mwaka 2019/20.

**Mchoro 4.8: Asilimia ya Kaya zilizounganishwa na Umeme wa ZECO kwa Eneo 2009/10 hadi 2019/20 Zanzibar HBS**




Matokeo pia yanaonesha kuwa uunganishaji wa umeme kaya zinazoongozwa na wanaume ni mkubwa (asilimia 56.9) ikilinganishwa na kaya zinazongozwa na wanawake (asilimia 50). Katika ngazi ya wilaya, wilaya ya Magharibi A ina zaidi ya asilimia 91 ya kaya zilizounganishwa na umeme, ikifuatiwa na wilaya ya Mjini asilimia 84.2, wilaya ya Magharibi B (asilimia 77.5), wilaya ya Micheweni ina asilimia ndogo ya kaya zilizounganishwa na umeme (asilimia 15.7). Kwa upande wa mwelekeo, wilaya zote zimeonesha mafanikio makubwa ya ongezeko la kaya zilizounganishwa na umeme katika kipindi cha miaka mitano **(Jedwali 4.1).**

**Jedwali 4. 1: Asilimia ya Kaya zilizounganishwa na Umeme kwa Jinsi na Wilaya, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS**

| Kipengele | 2014/15 | 2019/20 |
|---|---|---|
| **Jinsi ya Mkuu wa Kaya** | | |
| Mwanamme | 45.9 | 56.9 |
| Mwanamke | 37.9 | 50.3 |
| **Wilaya** | | |
| Kaskazini A | 18.3 | 25.7 |
| Kaskazini B | 19.1 | 35.5 |
| Kati | 25.4 | 34.4 |
| Kusini | 30.7 | 50.9 |
| Magharibi A | 67.8 | 91.4 |
| Magharibi B | | 77.5 |
| Mjini | 87.6 | 84.4 |
| Wete | 30.3 | 41.4 |
| Micheweni | 7.5 | 15.7 |
| Chake Chake | 41.3 | 54.8 |
| Mkoani | 15.3 | 28.9 |
| **Jumla** | **44.0** | **55.4** |

## 4.4 Matumizi ya Nishati

### 4.4.1 Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kuangazia

Kwa ujumla, umeme ni chanzo kikuu cha nishati ya kuangazia kwa kaya za Zanzibar. Matokeo yameonesha kuwa, kaya zaidi ya nusu (asilimia 55.3) ya zinztumiz nishati ya umeme kama ni chanzo kikuu cha kuangazia, maeneo ya mijini yana kaya zaidi zinazotumia umeme kwa kuangazia (asilimia 86.3) ikilinganishwa na kaya za vijijini (asilimia 32.8). Si jambo la kushangaza, matumizi ya mafuta ya taa kuwa ni chanzo kikuu cha kuangazia katika maeneo ya vijijini ambapo karibu kaya 5 kati ya kila kaya 10 zinatumia mafuta ya taa kwa kuangazia lakini kwa maeneo ya mijini ni asilimia 8 tu ya kaya zinatumia mafuta ya taa kwa kuangazia. Katika ngazi ya wilaya, Wilaya ya Micheweni (asilimia 66.4), Kaskazini A (asilimia 62.7), Mkoani (asilimia 53.7) na Kaskazini B (asilimia 52.1) zinaongoza kwa kutumia nishati ya mafuta ya taa kwa kuangazia.

Matumizi ya nishati ya umeme wa jua, wilaya ya Kati (asilimia 18.3), Micheweni (asilimia 14.3), Kusini (asilimia 14.1) na Mkoani (asilimia13.2) zinaongoza kwa kutumia nishati ya umeme wa jua kuwa ni chanzo kikuu cha nishati ya kuangazia **(Jedwali 4.2).**

**Jedwali 4. 2: Asilimia ya Kaya kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo, Wilaya na Aina ya Chanzo Kikuu cha Kuangazia 2019/20 Zanzibar HBS**

| Kipengele | Chanzo kikuu cha nishati ya kuangazia | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Umeme | Umeme wa Jua | Taa za chaji | Mafuta ya taa (Kibatari) | Kandili | Kuni | Nyingine | Jumla |
| **Jinsi ya Mkuu wa Kaya** | | | | | | | | |
| Mwanamme | 56.9 | 7.0 | 3.9 | 30.9 | 0.5 | 0.3 | 0.5 | 100.0 |
| Mwanawake | 50.3 | 4.5 | 3.9 | 39.6 | 0.5 | 0.4 | 0.8 | 100.0 |
| **Eneo** | | | | | | | | |
| Vijijini | 32.8 | 10.0 | 4.5 | 50.8 | 0.5 | 0.6 | 0.9 | 100.0 |
| Mijini | 86.3 | 1.5 | 3.1 | 8.5 | 0.5 | 0.0 | 0.1 | 100.0 |
| **Wilaya** | | | | | | | | |
| Kaskazini A | 25.7 | 5.9 | 4.9 | 62.7 | 0.0 | 0.8 | 0.0 | 100.0 |
| Kaskazini B | 35.5 | 8.4 | 2.6 | 52.1 | 0.4 | 0.0 | 1.0 | 100.0 |
| Kati | 34.4 | 18.3 | 11.4 | 32.3 | 1.8 | 0.0 | 1.9 | 100.0 |
| Kusini | 50.5 | 14.1 | 10.2 | 24.0 | 0.5 | 0.4 | 0.4 | 100.0 |
| Magharibi | 91.4 | 0.3 | 3.1 | 5.2 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 100.0 |
| Magharibi B | 77.5 | 3.5 | 3.5 | 14.1 | 0.5 | 0.0 | 0.9 | 100.0 |
| Mjini | 84.4 | 1.4 | 3.7 | 8.0 | 2.5 | 0.0 | 0.0 | 100.0 |
| Wete | 40.9 | 4.2 | 3.9 | 50.6 | 0.0 | 0.4 | 0.0 | 100.0 |
| Micheweni | 15.7 | 14.3 | 1.8 | 66.4 | 0.0 | 0.7 | 1.1 | 100.0 |
| Chake Chake | 54.8 | 4.1 | 1.9 | 38.3 | 0.0 | 0.5 | 0.4 | 100.0 |
| Mkoani | 28.9 | 13.2 | 2.0 | 53.7 | 0.0 | 1.1 | 1.2 | 100.0 |
| **Jumla** | **55.3** | **6.4** | **3.9** | **33.0** | **1.0** | **0.3** | **0.5** | **100.0** |

## 4.5 Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kupikia

Utafiti umeonesha kuwa, kuni bado ni chanzo kikuu cha nishati ya kupikia hapa Zanzibar, ambapo zaidi nusu (asilimia 54.7) ya kaya zinatumia kuni kwa kupikia, ikifuatiwa na mkaa (asilimia 33), gesi ya viwandani (asilimia 7.1) na umeme (asilimia 2.5). Matumizi ya kuni kwa kupikia ni makubwa kaya za vijijini (asilimia 80.9) ikilinganishwa na kaya katika maeneo ya mijini (asilimia 18.9). Kaya zinazoongozwa na wanawake zinatumia kuni kwa kupikia (asilimia 57.2) ikinganishwa na kaya zinazoongozwa na wanaume (asilimia 54).

Katika ngazi ya wilaya, wilaya ya Micheweni inaongoza kwa kuwa na kaya nyingi zaidi zinazotumia kuni kwa kupikia (asilimia 90.2) na matumizi ya gesi ya viwandani katika wilaya za Mjini, Magharibi A na Magharibi B zinaongoza zikiwa na asilimia 19.9, 15.2 na 11.4 kwa mtiririko **(Jedwali 4.3)**.

**Jedwali 4. 3: Asilimia ya Kaya kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo, Wilaya na Chanzo Kikuu Cha Nishati ya Kupikia, 2019/20 Zanzibar HBS**

| Kipengele | Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kupikia | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Umeme | Umeme wa Jua | Gesi | Kinyesi cha Wanyama | Mafuta ya Taa | Makaa ya Mawe | Mkaa | Kuni | Mbao/Field Residuals /Dust | Nyingine | Jumla |
| **Jinsi ya Mkuu wa Kaya** | | | | | | | | | | | |
| Mwanamke | 2.4 | 0.1 | 7.4 | 0.1 | 1.8 | 0.0 | 33.5 | 54.0 | 0.0 | 0.6 | 100.0 |
| Mwanamme | 2.5 | 0.2 | 6.4 | 0.1 | 2.0 | 0.1 | 31.2 | 57.2 | 0.0 | 0.2 | 100.0 |
| **Eneo** | | | | | | | | | | | |
| Vijijini | 1.1 | 0.2 | 2.2 | 0.1 | 2.0 | 0.0 | 13.0 | 80.9 | 0.0 | 0.6 | 100.0 |
| Mijini | 4.4 | 0.1 | 14.0 | 0.1 | 1.7 | 0.1 | 60.4 | 18.9 | 0.0 | 0.5 | 100.0 |
| **Wilaya** | | | | | | | | | | | |
| Kaskazini A | 0.6 | 0.0 | 0.9 | 0.0 | 3.4 | 0.0 | 10.6 | 84.1 | 0.0 | 0.4 | 100.0 |
| Kaskazini B | 0.3 | 0.0 | 2.1 | 0.0 | 2.4 | 0.0 | 9.4 | 85.8 | 0.0 | 0.0 | 100.0 |
| Kati | 0.0 | 0.0 | 4.7 | 0.0 | 2.1 | 0.0 | 6.3 | 85.2 | 0.0 | 1.7 | 100.0 |
| Kusini | 1.3 | 0.4 | 1.1 | 0.0 | 1.0 | 0.0 | 16.1 | 80.1 | 0.0 | 0.0 | 100.0 |
| Magharibi A | 5.1 | 0.0 | 15.2 | 0.0 | 2.8 | 0.0 | 59.8 | 16.6 | 0.1 | 0.5 | 100.0 |
| Magharibi B | 5.3 | 0.2 | 11.4 | 0.0 | 0.7 | 0.0 | 59.1 | 22.7 | 0.0 | 0.6 | 100.0 |
| Mjini | 5.2 | 0.3 | 19.9 | 0.5 | 2.4 | 0.5 | 55.7 | 15.6 | 0.0 | 0.0 | 100.0 |
| Wete | 1.5 | 0.0 | 1.4 | 0.0 | 0.6 | 0.0 | 27.1 | 68.5 | 0.0 | 0.9 | 100.0 |
| Micheweni | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.7 | 0.0 | 9.1 | 90.2 | 0.0 | 0.0 | 100.0 |
| Chake Chake | 0.0 | 0.7 | 1.9 | 0.0 | 1.7 | 0.0 | 27.7 | 67.4 | 0.0 | 0.5 | 100.0 |
| Mkoani | 0.5 | 0.0 | 0.6 | 0.3 | 2.1 | 0.0 | 10.7 | 84.6 | 0.0 | 1.2 | 100.0 |
| **Jumla** | **2.5** | **0.1** | **7.1** | **0.1** | **1.9** | **0.1** | **33.0** | **54.7** | **0.1** | **0.5** | **100.0** |

## 4.6 Vyanzo vya Maji

Matokeo yameonesha kupungua kwa matumizi ya maji katika vyanzo vilivyoimarishwa wakati wa kiangazi (asilimia 90.7) na kipindi cha mvua (asilimia 94.9) mwaka 2019/20 HBS. Licha kupungua katika kipindi cha kiangazi, wilaya nyingi za Zanzibar zinatumia maji kutoka katika vyanzo vilivyoimarishwa wakati wa kiangazi 2019/20HBS, isipokuwa wilaya ya Kati, na Micheweni **(Jedwali 4.4)**.

**Jedwali 4. 4: Asilimia ya kaya zenye Chanzo Kikuu cha Maji Kilichoimarishwa wakati wa Mvua na Kiangazi kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo na Wilaya 2019/20 Zanzibar HBS**

| | 2019/20 | |
|---|---|---|
| **Kipengele** | **Chanzo Kikuu cha Maji kilichoimarishwa wakati wakati wa Mvua** | **Chanzo Kikuu cha Maji Kilichoimarishwa wakati wa Kiangazi** |
| **Jinsi ya Mkuu wa Kaya** | | |
| Mwanamme | 94.8 | 90.2 |
| Mwanamke | 95.5 | 92.5 |
| **Eneo** | | |
| Vijijini | 98.6 | 88.3 |
| Mijini | 94.9 | 96.6 |
| **Wilaya** | | |
| Kaskazini A | 98.6 | 96.8 |
| Kaskazini B | 98.7 | 98.1 |
| Kati | 89.3 | 83.9 |
| Kusini | 95.0 | 90.8 |
| Magharibi A | 99.3 | 98.6 |
| Magharibi B | 97.8 | 95.4 |
| Mjini | 100.0 | 100.0 |
| Wete | 98.4 | 98.0 |
| Micheweni | 46.2 | 37.1 |
| Chake Chake | 98.7 | 97.2 |
| Mkoani | 92.2 | 89.3 |
| **Jumla** | **94.9** | **90.7** |

## 4.7 Huduma ya Vyoo

Kiwango cha kaya zenye vyoo kimeongezeka kutoka asilimia 83.7 mwaka 2014/15 hadi kufikia asilimia 87.5 mwaka 2019/20. Kaya zinazoongozwa na wanaume zina idadi kubwa zaidi ya huduma ya vyoo ikilinganishwa na kaya zinazongozwa na wanawake. Ukitoa Mkoani ambayo haikuwa na mabadiliko, wilaya zote zimeonesha mabadiliko katika kiwango cha kaya zilizo na vyoo. **(Jedwali 4.5)**.

**Jedwali 4. 5: Asilimia ya Kaya zenye Aina yoyote ya Choo, Zisizo na Choo kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo na Wilaya, Zanzibar 2014/15 and 2019/20 HBS**

| Kipengele | 2014/15 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kaya zenye huduma ya Choo | Kaya Zisizo naa choo | Jumla | Kaya zenye huduma ya Choo | Kaya Zisizo naa choo | Jumla |
| **Jinsi ya Mkuu wa Kaya** | | | | | | |
| Mwanamme | 84.7 | 15.3 | 100.0 | 88.6 | 11.4 | 100.0 |
| Mwanamke | 80.2 | 19.8 | 100.0 | 83.9 | 16.1 | 100.0 |
| **Eneo** | | | | | | |
| Vijini | 72.5 | 27.5 | 100.0 | 78.9 | 21.1 | 100.0 |
| Mijini | 98.3 | 1.7 | 100.0 | 99.3 | 0.7 | 100.0 |
| **Wilaya** | | | | | | |
| Kaskazini A | 82.0 | 18.0 | 100.0 | 91.4 | 8.6 | 100.0 |
| Kaskazini B | 80.8 | 19.2 | 100.0 | 90.8 | 9.2 | 100.0 |
| Kati | 92.9 | 7.1 | 100.0 | 94.1 | 5.9 | 100.0 |
| Kusini | 92.0 | 8.0 | 100.0 | 95.8 | 4.2 | 100.0 |
| Mjini | 99.9 | 0.1 | 100.0 | 100.0 | 0 | 100.0 |
| Magharibi A | 99.1 | 0.9 | 100.0 | 99.7 | 0.3 | 100.0 |
| Magharibi B | | | | 99.9 | 0.1 | 100.0 |
| Wete | 60.7 | 39.3 | 100.0 | 76.3 | 23.7 | 100.0 |
| Micheweni | 38.0 | 62.0 | 100.0 | 44.5 | 55.5 | 100.0 |
| Chake Chake | 71.3 | 28.7 | 100.0 | 82.4 | 17.6 | 100.0 |
| Mkoani | 65.8 | 34.2 | 100.0 | 64.6 | 35.4 | 100.0 |
| **Jumla** | **83.7** | **16.3** | **100.0** | **87.5** | **12.5** | **100.0** |

## 4.8 Umiliki wa Akaunti za Benki

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa idadi ya kaya zenye angalau mwanakaya mmoja mwenye akaunti ya benki imeongezeka kutoka asilimia 17.8 mwaka 2014/15 hadi kufikia asilimia 27.7 mwaka 2019/20 **(Jedwali 4.6)**. Kiwango cha kaya za vijijini zenye angalau mwanakaya mmoja mwenye akaunti ya benki zimeongezeka kutoka asilimia 10.2 mwaka 2014/15 hadi kufikia asilimia 15.9 mwaka 2019/20. Hii inatokana na mipango na mageuzi ya utekelezaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar(PBZ) za kupanua huduma zake. Vile vile, idadi ya kaya zinazongozwa na wanawake ambao wana angalau mwanakaya mmoja mwenye akaunti ya benki zimeendelea kukua, ingawa bado kaya zinazoongozwa na wanaume zenye angalau mwanakaya mmoja mwenye akaunti ya benki zinaongoza.

Matokeo kiwilaya yameonesha kuwa, Idadi ya kaya zenye angalau mwanakaya mmoja mwenye akaunti ya benki takriban wilaya zote imeongezeka isipokuwa wilaya Mkoani.

**Jedwali 4. 6: Asilimia ya Kaya zenye angalau Mwanakaya mmoja mwenye Akaunti ya Benki kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo na Wilaya, 2014/15 na 2019/20 Zanzibar HBS**

| Kipengele | 2014/15 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Angalau mwanakaya mmoja ana Akaunti ya Benki | Hakuna mwanakaya mwenye Akaunti ya Benki | Jumla | Angalau Mwanakaya mmoja mwenye Akaunti ya Benki | Hakuna Mwanachama mwenye Akaunti ya Benki | Jumla |
| **Jinsi ya Mkuu wa Kaya** | | | | | | |
| Mwanamme | 19.4 | 80.6 | 100.0 | 29.4 | 70.6 | 100.0 |
| Mwanamke | 12.5 | 87.5 | 100.0 | 22.2 | 77.8 | 100.0 |
| **Eneo** | | | | | | |
| Vijijini | 10.2 | 89.8 | 100.0 | 15.9 | 84.1 | 100.0 |
| Mijini | 27.9 | 72.1 | 100.0 | 43.9 | 56.1 | 100.0 |
| **Wilaya** | | | | | | |
| Kaskazini A | 8.8 | 91.2 | 100.0 | 12.6 | 87.4 | 100.0 |
| Kaskazini B | 7.1 | 92.9 | 100.0 | 12.6 | 87.4 | 100.0 |
| Kati | 12.6 | 87.4 | 100.0 | 15.3 | 84.7 | 100.0 |
| Kusini | 8.2 | 91.8 | 100.0 | 22.8 | 77.2 | 100.0 |
| Mjini | 32.5 | 67.5 | 100.0 | 47.8 | 52.2 | 100.0 |
| Magharibi A | 25.3 | 74.7 | 100.0 | 32.9 | 67.1 | 100.0 |
| Magharibi B | | | | 48.7 | 51.3 | 100.0 |
| Wete | 11.1 | 88.9 | 100.0 | 19.1 | 80.9 | 100.0 |
| Micheweni | 4.6 | 95.4 | 100.0 | 7.5 | 92.5 | 100.0 |
| Chake chake | 20.4 | 79.6 | 100.0 | 38.2 | 61.8 | 100.0 |
| Mkoani | 9.2 | 90.8 | 100.0 | 7.4 | 92.6 | 100.0 |
| **Jumla** | **17.8** | **82.2** | **100.0** | **27.7** | **72.3** | **100.0** |



